# YALIYOMO


Yaliyomo.........1
Dibaji.........2
Dira na Dhima ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe.........3
Vifupisho vya Maneno.........4
Ramani ya Wilaya ya Mbogwe.........5
Tamko la Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya.........6
1.0 Utangulizi.........8
1.1 Shughuli za Kiuchumi na Pato la Wilaya ya Mbogwe.........8
2.0 Utekelezaji wa Ahadi za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.........9
2.1 Ahadi: Kujenga Barabara ya Lami katika Mji wa Masumbwe (Km 3).........9
2.1.1 Utekelezaji wa Ahadi.........9
3.0 Vipaumbele vya Wilaya ya Mbogwe.........9
3.1 Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe.........9
3.1.1 Huduma za Kijamii.........9
3.1.1.1 Utumishi na Utawala Bora.........9
3.1.1.1.1 Idadi ya Watumishi.........9
3.1.1.1.2 Ujenzi wa ofisi na nyumba za watumishi.........10
3.1.1.1.3 Vitendea kazi (Huduma ya magari).........11
3.1.1.2 Elimu.........12
3.1.1.2.1 Elimu Msingi.........12
3.1.1.2.1.1 Ongezeko la wanafunzi.........13
3.1.1.2.1.2 Elimu Bure.........13
3.1.1.2.1.3 Hali ya Miundombinu.........13
3.1.1.2.2 Elimu Sekondari.........17
3.1.1.2.2.1 Ongezeko la wanafunzi.........17
3.1.1.2.2.2 Elimu Bure.........18
3.1.1.2.2.3 Hali ya Miundombinu.........18
3.1.1.2.2.4 Ujenzi wa Kidato cha 5 na 6.........22
3.1.1.3 Afya na Ustawi wa Jamii.........24
3.1.1.3.1 Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya.........24
3.1.1.3.2 Ujenzi wa vituo vya afya na zahanati.........25
3.1.1.3.3 Mafanikio ya jumla sekta ya afya.........27
3.1.1.3.4 Dawa, Vifaa tiba na Vitendanishi.........28
3.1.1.4 Ujenzi wa stendi ya mabasi.........28
3.1.2 Huduma za Kiuchumi.........29
3.1.2.1 Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika.........30
3.1.2.2 Mifugo na Uvuvi.........32
3.1.2.3 Ardhi na Maliasili.........33
3.1.3 Uwezeshaji wananchi kiuchumi.........35
3.1.3.1 Maendeleo ya Jamii.........35
3.1.3.2 Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).........36
3.1.3.3 Mwenendo wa Makusanyo ya fedha.........38
3.2 Idara na Taasisi zingine za Serikali.........40
3.2.1 TANESCO.........40
3.2.2 TARURA.........43
3.2.3 TFS.........49
3.2.4 RUWASA.........50
4.0 Fursa za Uwekezaji Wilaya ya Mbogwe.........55

# DIBAJI

Kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Mbogwe napenda kutumia nafasi hii kukishukuru na kukipongeza Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa kuandaa vizuri ilani yake ya Uchaguzi ya mwaka 2015 na kuisimamia Serikali kutekeleza Ahadi zilizomo katika ilani hii; Aidha, kipekee nimshukuru sana Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Taifa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika juhudi zake za kuleta maendeleo katika Taifa letu hususani ukusanyaji wa mapato, kukemea ufisadi na matumizi mabaya ya fedha za umma. Wananchi wana imani na matumaini makubwa na uongozi wake, na wanamtakia kila la kheri katika shughuli za kuliongoza Taifa. Aidha, ahadi za Mhe. Rais zimekuwa zikitekelezwa mwaka hadi mwaka kwa asilimia 100 jambo ambalo linawapa matumaini na kuleta imani kwa wananchi wa Wilaya ya Mbogwe kwa Chama chao Tawala.



Martha J. Mkupasi
**MKUU WA WILAYA MBOGWE**

Wilaya ya Mbogwe iliyoko Kaskazini Magharibi mwa Tanzania ni moja kati ya Halmashauri sita (6) zinazounda Mkoa wa Geita, ambayo ilianzishwa tarehe 9/05/2012 kutoka Wilaya mama ya Bukombe katika Mkoa wa Geita na kutangazwa katika Gazeti la Serikali na kupewa Tangazo la Serikali GN (Governmet Notes) 286. Lengo la serikali kuanzisha Wilaya hii ni kuchochea maendeleo na kusogeza huduma za utawala karibu na wananchi.

Tumepakana na Wilaya za Geita na Chato upande wa Kaskazini Magharibi, upande wa Kaskazini Mashariki inapakana na Wilaya ya Nyang'hwale, upande wa Mashariki inapakana na Wilaya ya Kahama Mkoa wa Shinyanga na upande wa Magharibi inapakana na Wilaya ya Bukombe, upande wa kusini inapakana na pori la Hifadhi la Kigosi Muyobosi. Kwasasa ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe na ofisi ya Mkuu wa Wilaya ziko katika Mji wa Masumbwe barabara kuu itokayo Kahama kwenda nchi za Burundi, Uganda, DRC na Rwanda.

Taarifa hii inaelezea mafanikio ya Ilani ya CCM yaliyopatikana kwa kipindi cha mwaka 2015 – 2020 Chini ya Dkt. John Pombe Joseph Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imezingatia maeneo mbalimbali kama yalivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi kwa kufuata Ibara. Aidha, Pamoja na Changamoto mbalimbali zilizojitokea Wilaya imeendelea kusimamia na kutekeleza shughuli majukumu yake kama yalivyoainishwa katika Ilani ya CCM kwa kipindi cha mwaka 2015-2020.

Martha J. Mkupasi
**MKUU WA WILAYA**
**MBOGWE**

**DIRA NA DHIMA YA HALMASHAURI YA WILAYA YA MBOGWE**

**DIRA YA HALMASHAURI**

"KUWA HALMASHAURI BORA KWA KUBORESHA HUDUMA ZA KIJAMII NA KIUCHUMI"

**DHIMA YA HALMASHAURI**

"KUHAKIKISHA WANANCHI WOTE WANAPATA HUDUMA BORA ZA KIJAMII NA KIUCHUMI KWA KUTUMIA FURSA NA RASILIMALI ZILIZOPO KWA KUZINGATIA USAWA, JINSIA NA UTAWALA WA SHERIA".



MHE. VICENT B. BUSIGA

MWENYEKITI WA HALMASHAURI
**MBOGWE**

**MAENEO MAKUU YENYE MATOKEO (KEY RESULTS AREAS)**

1. KUIMARISHA UCHUMI ENDELEVU
2. HUDUMA BORA ZA KIUCHUMI NA KIJAMII
3. USHIRIKI WA JAMII KATIKA KUBAINISHA NA KUTEKELEZA VIPAUMBELE VYA MAENDELEO KATIKA WILAYA
4. UFANISI WA MATUMIZI YA RASILIMALI ZA UMMA
5. UTEKELEZAJI WA UTAWALA BORA
6. KUIMARISHA ULINZI NA USALAMA
7. KUIMARISHA USAFI NA MAZINGIRA
8. USIMAMIZI WA FEDHA NA UWAJIBIKAJI
9. KUENDELEZA RASILIMALI WATU

VICENT B. BUSIGA
MWENYEKITI WA HALMASHAURI
**MBOGWE**

## VIFUPISHO VYA MANENO

TARURA – Tanzania Rural and Urban Roads Agency

AGPAHI - Ariel Glaser Pediatric AIDS Healthcare Initiative

CAG - Controller and Auditor General

CDCF - Constituencies Development Catalyst Fund

CSSC- Christian Social Services Commission

DADPs - District Agricultural Development Plans

EGPAF- Elizabeth Glaser Pediatric AIDS Healthcare Foundation

GPG - General Purpose Grants

HSBF - Health Sector Basket Fund

LAAC - Local Authorities Accounts Committee

LGCDG - Local Government Capital Development Grants

MMAM - Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi

NHIF - National Health Insurance Fund

NMSF - National Multi-Sectoral Strategic Framework

RWSSP - Rural Water Supply and Sanitation Project

TACAIDS - Tanzania Commission for AIDS

TASAF -Tanzania Social Action Fund

TZS -Tanzania Shillings

WYDF - Women and Youth Development Fund


GGM – Geita Gold Mines

CSR – Community Social Responsibility

TEA – Tanzania Education Authority

EP4R – Education Performance For Results

# MBOGWE DISTRICT MAP-WARDS BOUNDARIES



## TAMKO LA MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI



Elias M. Kayandabila
Mkurugenzi Mtendaji (W)
**MBOGWE**

Nitumie fursa hii kuishukuru Serikali, Sekretarieti ya Mkoa wa Geita, viongozi wa Chama Cha Mapinduzi Wilaya ya Mbogwe, Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Mbogwe, Mbunge wa Jimbo la Mbogwe, Madiwani na Wakuu wa Idara na Vitengo kwa mshikamano na kupata mafanikio haya.

Katika Kipindi cha Mwaka 2015-2020 Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe imefanikiwa kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo hususan, sekta za Elimu, Utawala, Maji, Barabara na Afya ambapo takribani kiasi cha fedha shilingi bilioni 26.3 zimepokelewa na kutumika katika jitihada za serikali za kuwahudumia wananchi wa Wilaya ya Mbogwe.

Katika kipindi tajwa vyanzo vipya vya mapato vimeanzishwa ili kuiwezesha Halmashauri kujitegemea. Tumeanzisha mradi wa stendi ya mabasi eneo la Mzambarauni ambao uko hatua ya ukamilishaji, Soko la Dhahabu, Halmashauri imeunda kikosi kazi cha ukusanyaji wa mapato ambacho kimeweza kufanikiwa kukusanya mapato kwa ufanisi. Aidha, katika mwaka wa fedha 2019/2020 hadi kufikia Mei, 2020 Halmashauri imefanikiwa kukusanya jumla ya Tshs. 919,029,762.2 sawa na asilimia 101 ya lengo la mwaka haya ni mafanikio makubwa sana ukilinganisha na miaka iliyopita.

Halmashauri ya Wilaya pamoja na changamoto ambazo imekumbana nazo katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kama vile ukame na upungufu wa watumishi bado imeweza kutekeleza miradi yake kwa ufanisi na kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani. Kwa Mujibu wa taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Halmashauri yetu imeendelea kupata Hati safi za ukaguzi kwa miaka miwili mfululizo kuanzia mwaka 2017/2018 hadi 2018/2019.

Aidha, mwanzoni mwa mwezi Juni, 2020 Halmashauri imepokea kiasi cha shilingi Milioni 500 fedha za ujenzi wa hospitali ya Wilaya ambapo ujenzi wake uko hatua ya kujenga msingi; tumefanya ukarabati wa vituo viwili vya afya Iboya na Masumbwe kwa shilingi Milioni 800 kwa kujenga wodi mbili, chumba cha kuhifadhia maiti, nyumba ya mtumishi na maabara katika vituo hivyo; tumejenga miundombinu ya elimu msingi na sekondari kwa kujenga vyumba vya madarasa, nyumba za walimu, mabweni na vyoo vya walimu na wanafunzi; tumefanikiwa kuendelea kujenga jengo la Utawala ofisi za Halmashauri ya Wilaya kwa awamu ya kwanza (Phase one) ambapo utekelezaji wake uko hatua ya ukamilishaji.

Kutokana na miradi mingi kutumia vikundi (Force account) kumesababisha kuokoa gharama nyingi kwenye miradi ya ujenzi, Mafanikio haya yametokana na ushirikiano mkubwa kuanzia kwa Mhe. Mkuu wa Wilaya na Kamati yake ya Ulinzi na Usalama, Madiwani, Wakuu wa idara na Vitengo, watumishi wa makao makuu hadi ngazi za vijiji, Maafisa Tarafa pamoja na viongozi wote waliopo katika ngazi ya vijiji na vitongoji.

Elias M. Kayandabila
Mkurugenzi Mtendaji (W)
**MBOGWE**

## 1.0 UTANGULIZI

Wilaya imegawanywa katika tarafa 3 ambazo ni Masumbwe, Ilolangulu na Mbogwe. Aidha, Wilaya ina kata 17, vijiji 87 na vitongoji 335. Inakadiriwa kuwa na ukubwa wa kilomita za mraba 3,677 sawa na hekta 367,418 ambapo hekta 2,143.69 sawa na asilimia 58.3 hutumika kwa shughuli za makazi, kilimo na ufugaji na hekta 1,533.31 sawa na asilimia 41.7 ni eneo la hifadhi. Shughuli kuu za kiuchumi ni kilimo, ufugaji wa mifugo, ufugaji wa nyuki, uchimbaji mdogo mdogo wa madini, ajira rasmi na zisizo rasmi na sekta binafsi.

Kwa Mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012, Wilaya ya Mbogwe ilikuwa na jumla ya watu 193,922, wanawake wakiwa ni 98,839 na wanaume 95,083. Kiwango cha ongezeko la watu ni 6.4%. Hivi sasa Wilaya inakadiriwa kuwa na watu 258,460, wanawake wakiwa ni 131,293 na wanaume 127,167. Ongezeko linachangiwa na kuzaana (55%) na uhamiaji kutokana na uchimbaji mdogo mdogo wa madini (45%). Wastani wa ukubwa wa kaya ni asilimia 6.4.

Wilaya inakadiriwa kuwa na watu 97,888 wenye uwezo wa kufanya kazi (nguvu kazi), sawa na silimia 50 ya idadi ya watu wote kwa sasa. Hali ya Hewa ya Wilaya ni ya ki-tropiki, wastani wa joto ni $22^0$ C na wastani wa mvua kwa mwaka ni kati ya 900mm – 1200mm.

### 1.1 SHUGHULI ZA KIUCHUMI NA PATO LA WILAYA

Wakazi wa Wilaya ya Mbogwe wanajishughulisha na shughuli mbalimbali za kilimo kinachochangia takribani asilimia 75 ya pato la Wilaya, wakati shughuli zingine za kiuchumi zinachangia asilimia 25. Pato la wananchi ni la chini kifedha. Asilimia Sabini na Tisa (79) ya wakazi wanaishi chini ya dola 1 kwa siku.

## 2.0 UTEKELEZAJI WA AHADI ZA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA ALIZOZITOA MWAKA 2015 KATIKA WILAYA YA MBOGWE

Akiwa Mgombea Urais kwa Tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitoa ahadi wakati wa Kampeni za Uchaguzi Mkuu katika Wilaya ya Mbogwe mwaka 2015, jitihada za kutekeleza ahadi hii ni kama ifuatavyo:

### 2.1 Ahadi: Kujenga Barabara ya Lami katika Mji wa Masumbwe (Km 3)

**2.1.1 Utekelezaji wa Ahadi:** Ujenzi wa Km 1.2 uko hatua za ukamilishaji na unatarajia kukamilika tarehe 30 Julai, 2020. Ujenzi wa Km 1.8 unatarajia kuanza mwaka wa fedha 2020/21 mwezi Julai, 2020 na unatarajia kukamilika mwezi Septemba, 2020.

## 3.0 VIPAUMBELE VYA WILAYA YA MBOGWE

Wilaya ya Mbogwe ilipanga kutekeleza shughuli zitakazotekelezwa katika kipindi cha miaka 5 (2015-2020) kwa kuzingatia MKUKUTA na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025. Wilaya imejiwekea vipaumbele kama ifuatavyo:- Kuboresha miundombinu ya Elimu, Afya, Kilimo, Mifugo, Maendeleo ya watumishi, huduma za afya, Mapambano dhidi ya UKIMWI, Barabara na Maji. Utekelezaji wa vipaumbele hivi umejikita katika Taasisi za Serikali kama vile Halmashauri, TANESCO, TARURA na RUWASA kama ifuatavyo:

### 3.1 HALMASHAURI YA WILAYA YA MBOGWE

Halmashauri imejiwekea vipaumbele vinavyozingatia huduma za jamii, huduma za kiuchumi na uwezeshaji wananchi kiuchumi kama ifuatavyo:-

#### 3.1.1 HUDUMA ZA KIJAMII

##### 3.1.1.1 UTUMISHI NA UTAWALA BORA

**ILANI YA CHAMA CHA MAPINDUZI** ya mwaka 2015 Ibara ya 145, inasema Chama Cha Mapinduzi kitaielekeza Serikali kuendeleza Utawala Bora, Demokrasia na Uwajibikaji; Wilaya ya Mbogwe katika kutekeleza ibara hii imetekeleza kama ifuatavyo:

###### 3.1.1.1.1 IDADI YA WATUMISHI

- Kwa kipindi cha mwaka 2015-2020 Halmashauri imepata mafanikio makubwa ya ongezeko la watumishi katika kada mbalimbali ambapo mwaka 2015 ilikuwa na watumishi 1,465 hadi kufikia mwaka 2020 ilikuwa na watumishi 1,671 kati ya watumishi 2,345 wanaohitajika, sawa na ongezeko la asilimia 12. Watumishi hawa wanatoa huduma katika idara kumi na mbili (12) ambazo ni Utawala, Mipango & Biashara, Fedha, Elimu, Ujenzi, Ardhi, Maliasili & Mazingira, Maendeleo ya Jamii, Kilimo, Mifugo & Ushirika, Maji, Afya pamoja na vitengo vitano (5) ambavyo ni Sheria, Ukaguzi wa ndani, Uchaguzi, Nyuki na Tehama.

### 3.1.1.1.2 UJENZI WA OFISI ZA HALMASHAURI NA NYUMBA ZA WATUMISHI

- Kupitia fedha Maalumu za Ujenzi wa Ofisi za Halmashauri na nyumba za watumishi, Wilaya imefanikiwa kujenga Ofisi za Halmashauri, ujenzi wake uko katika hatua za ukamilishaji na kujenga nyumba sita za watumishi awamu ya kwanza katika hatua ya maboma; Ambapo kwa kipindi cha Mwaka 2015-2020 kiasi cha **Shilingi.2,140,102,798** zimepokelewa na kutumika katika miradi hiyo.



**Kampuni ya TTCL Wakifunga Mkongo wa Taifa ofisi za Halmashauri ya Wilaya**



**Muonekano wa Ujenzi wa Ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe**



**Muonekano wa Ujenzi wa nyumba za watumishi**

### 3.1.1.1.3 VITENDEA KAZI (HUDUMA YA MAGARI)

- Kwa kipindi cha Mwaka 2015-2020 Halmashauri ya Wilaya imepata mafanikio makubwa ya ongezeko la magari ya matumizi ya ofisi ambapo magari yameongezeka kutoka magari 9 mwaka 2015 hadi magari 18 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 50.



**Gari ya Mkurugenzi Mtendaji: Mkurugenzi akikabidhiwa gari Ofisi ya Rais – Ikulu**




**Baadhi ya magari ya ofisi ambayo hutumika kuhudumia wananchi**

### 3.1.1.2 ELIMU

**ILANI YA CHAMA CHA MAPINDUZI** ya mwaka 2015 Ibara ya 52 (a) inaelekeza: Elimu ya kisasa na hasa yenye muelekeo wa sayansi na Teknolojia ina nafasi ya pekee katika kufanikisha ujenzi wa msingi wa uchumi wa kisasa wa Taifa linalojitegemea. Kwa kutambua ukweli huu CCM inaipa kipaumbele sekta ya Elimu umuhimu wa kipekee ili kuiendeleza sekta hii. "Katika kipindi cha miaka mitano (2015 - 2020) CCM ilihakikisha serikali inasimamia utekelezaji wa sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014". Kufuatia mkakati huo Halmashauri ya Wilaya imepata mafanikio kama ifuatavyo:

#### 3.1.1.2.1 ELIMU MSINGI

- Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe ina jumla ya shule 92, shule 86 za Serikali na shule 6 ni Binafsi. Shule za Msingi za Serikali zina jumla ya wanafunzi 75,443 wakiwemo wavulana 37,404 na wasichana 38,039 kwa madarasa ya awali hadi darasa la VII.

#### 3.1.1.2.1.1 ONGEZEKO LA WANAFUNZI SHULE ZA MSINGI

- Idadi ya wanafunzi wa Elimu ya msingi imeongezeka kutoka 40,044 mwaka 2015 hadi 75,443 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 88.4.

#### 3.1.1.2.1.2 ELIMU BURE

- Kwa kipindi cha mwaka 2015-2020 Halmashauri imefanikiwa kupokea na kutumia kiasi cha **Shilingi. 2,091,656,786** kwa ajili ya elimu bure kwa shule za Msingi ili kuboresha huduma za elimu kwa wanafunzi wa Wilaya ya Mbogwe.

#### 3.1.1.2.1.3 HALI YA MIUNDOMBINU

- Katika kipindi cha mwaka 2015-2020 Halmashauri ya Wilaya kwa kushirikiana na Serikali Kuu, Wadau na wananchi imefanikiwa kuongeza madarasa, matundu ya vyoo, nyumba za walimu na madawati.

**(i) Ujenzi wa vyumba vya Madarasa na Ofisi**

- Idadi ya madarasa ya Elimu ya Msingi yameongezeka kutoka 580 mwaka 2015 hadi 674 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 16.2.

- Halmashauri imefanikiwa kupaua na kuezeka vyumba 42 vya madarasa ya shule za msingi kupitia ufadhili wa fedha za Community Social Responsibility (CSR) kutoka mgodi wa Geita Gold Mines (GGM), Kujenga vyumba vya madarasa katika shule ya msingi Kasandalala (Ufadhili wa fedha za TEA), Ukamilishaji wa vyumba 18 vya madarasa na ofisi 10 za walimu katika shule ya Muungano, Lubeho, Kisumo, Bugomba, Majengo, Iponya, Nhomolwa, Igalula, Mwagimagi, Kabanga na Songambele (Ufadhili wa fedha za Education Performance For Results - EP4R). Jumla ya **Shilingi. 337,200,000** zilitumika kuwezesha shughuli hizo.





**Muonekano wa vyumba vya madarasa shule ya msingi Mwagimagi**



**Muonekano wa vyumba vya madarasa na vyoo shule ya msingi Kabanga**




**Muonekano wa vyumba vya madarasa shule ya msingi Kasandalala**



**Muonekano wa shule ya elimu awali na msingi ya Ave Maria Shinyanga"A"**

**Muonekano wa miradi iliyofadhiliwa na Kampuni ya Mgodi wa dhahabu Geita (GGM) kupitia fedha za CSR – Kupaua Vyumba Vya Madarasa Shule Za Msingi**



**SHULE YA MSINGI MUUNGANO**



**SHULE YA MSINGI ILOLANGULU**



**SHULE YA MSINGI UHURU**

- Katika kuboresha miundombinu ya shule za msingi hususan ujenzi wa vyumba vya madarasa, Mkuu wa Wilaya ya Mbogwe kwa kushirikiana na ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe ameendelea kuhamasisha wananchi katika ujenzi wa vyumba vya madarasa ambapo hadi tarehe 30 Juni, 2020 vyumba 293 vilikuwa vimejengwa vikiwa katika hatua mbalimbali ya utekelezaji, kati ya idadi hiyo vyumba 88 vimekamilika, vyumba 24 viko hatua ya ukamilishaji, vyumba 13 viko hatua ya upauaji, vyumba 91 viko hatua ya lenta, vyumba 38 viko hatua ya boma, vyumba 10 misingi bado kukamilika na vyumba 39 misingi yake imekamilika.

- Mfano mzuri wananchi wa kijiji cha Shinyanga B wamejiwekea lengo la kujenga vyumba 22 vya madarasa katika shule ya msingi Kasandalala kwa nguvu zao ambapo hadi tarehe 30 Juni, 2020 vyumba 6 vya madarasa vilikuwa hatua ya boma, vyumba 8 vya madarasa viko hatua ya lenta na vyumba 8 vya madarasa viko hatua ya msingi.



**Muonekano wa ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule ya msingi Kasandalala**

### (ii) Ujenzi wa nyumba za walimu

- Idadi ya nyumba za walimu wa shule za Msingi imeongezeka kutoka nyumba 287 mwaka 2015 hadi nyumba 294 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 4.5. Halmashauri imefanikiwa kukamilisha nyumba 5 za walimu katika shule ya Itimbya, Nhomolwa, Busabaga, Isenengeja na Songambele (Ufadhili wa fedha za EP4R). Jumla ya **Shilingi. 93,000,000** zilitumika kuwezesha shughuli hizo.

### (iii) Ujenzi wa Matundu ya vyoo

- Idadi ya matundu ya vyoo imeongezeka kutoka 287 mwaka 2015 hadi 709 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 147.

### (iv) Idadi ya Madawati

- Idadi ya madawati ya Elimu msingi imeongezeka kutoka 9,683 mwaka 2015 hadi 18,153 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 87.5.

### (v) Idadi ya walimu

- Idadi ya walimu wa Elimu ya msingi imeongezeka kutoka 866 mwaka 2015 hadi 920 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 6.

### (vi) Uandikishaji wa darasa la kwanza

- Uandikishaji wa darasa la kwanza umeongezeka kutoka 8,797 mwaka 2015 hadi 11,129 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 27.

### (vii) Uwiano wa kitabu na wanafunzi

- Uwiano wa kitabu na wanafunzi umeongezeka kutoka 1:3 mwaka 2015 hadi 1:4 mwaka 2020.

#### 3.1.1.2.2 ELIMU SEKONDARI

- Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe ina jumla ya shule 16 za Sekondari za Serikali za kawaida (O'level) zenye usajili rasmi.

##### 3.1.1.2.2.1 ONGEZEKO LA WANAFUNZI SHULE ZA SEKONDARI

- Idadi ya wanafunzi wanaojiunga na kidato cha kwanza imeongezeka kutoka 1,770 mwaka 2015 hadi 3,011 mwaka 2020 sawa na asilimia 70.

- Idadi ya wanafunzi waliofaulu kidato cha pili imeongezeka kutoka 821 mwaka 2015 hadi 1,005 mwaka 2020 sawa na asilimia 22.

- Idadi ya wanafunzi waliofaulu kidato cha nne imeongezeka kutoka 344 mwaka 2015 hadi 2,019 sawa na asilimia 486.

- Idadi ya wanafunzi wanaojiunga na elimu ya kidato cha 5 imeongezeka kutoka kutoka 157 mwaka 2015 hadi 233 sawa na asilimia.

#### 3.1.1.2.2.2 ELIMU BURE

- Kwa kipindi cha mwaka 2015-2020 Halmashauri imefanikiwa kupokea na kutumia kiasi cha **Shilingi. 1,413,222,332** kwa ajili ya elimu bure kwa shule za Sekondari ili kuboresha huduma za elimu kwa wanafunzi wa Wilaya ya Mbogwe.

#### 3.1.1.2.2.3 HALI YA MIUNDOMBINU

**(i) Idadi ya shule za sekondari**

- Idadi ya shule za sekondari imeongezeka kutoka 13 mwaka 2015 hadi 16 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 23.

**(ii) Ujenzi wa vyumba vya Madarasa**

- Idadi ya vyumba vya madarasa ya Elimu ya Sekondari imeongezeka kutoka 103 mwaka 2015 hadi 160 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 55.

- Kupitia fedha za Benki ya Dunia (World Bank) Wilaya imefanikiwa Kujenga vyumba vinne vya madarasa, vyoo vya wanafunzi na walimu na nyumba ya walimu (Six in One) shule ya sekondari Iponya ambapo Jumla ya **Shilingi. 288,567,265** zilitumika kuwezesha shughuli hizo.

- Kupitia fedha za EP4R, Fedha za ukamilishaji wa Maboma na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), Halmashauri imefanikiwa kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa na katika shule ya Lulembela, Ikobe, Ikunguigazi, Ilolangulu, Iponya, Isangijo, Masumbwe, Nhomolwa, Nyakasaluma, Isebya, Ngemo, Nanda na Mbogwe ambapo Jumla ya **Shilingi. 752,811,492** zilitumika kuwezesha shughuli hizo.




**Muonekano wa vyumba vya madarasa shule ya sekondari Nanda**




**Muonekano wa vyumba vya madarasa shule ya sekondari Masumbwe**

**JITIHADA ZA WANANCHI KUJENGA VYUMBA VYA MADARASA**

- Katika kuboresha miundombinu ya shule za sekondari hususan ujenzi wa vyumba vya madarasa, Mkuu wa Wilaya ya Mbogwe kwa kushirikiana na ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe ameendelea kuhamasisha wananchi katika ujenzi wa vyumba vya madarasa mfano mzuri wananchi wa kata ya Masumbwe walijiwekea lengo la kujenga vyumba 10 vya madarasa, mabweni mawili na bwalo moja katika shule ya sekondari Nyakasaluma hadi tarehe 30 Juni, 2020 ujenzi wa misingi umekamilika na ufyatuaji wa tofali za Mfungamano unaendelea na uchimbaji wa Mashimo ya bwalo ya nguzo unaendelea.

- Katika kuboresha miundombinu ya shule za sekondari wananchi wa kata ya Lugunga wameamua kujenga shule mpya ya sekondari inayojengwa katika kijiji cha Kakumbi lengo wawe na shule 2, ambapo wamejiwekea malengo ya kujenga vyumba 2 vya madarasa, vyumba 2 vya maabara, nyumba 1 ya mwalimu na jengo la utawala; Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020 utekelezaji wake ulikuwa kama ifuatavyo:- Jengo la utawala liko hatua ya boma, vyumba vya madarasa na maabara maboma yake yamekamilika yanasubiri upauaji na nyumba ya mwalimu iko hatua ya maandalizi ya kurekebisha msingi.

- Wananchi wa kata ya Bunigonzi wameamua kujenga shule tarajali ya sekondari katika kata yao kwakuwa kata yao haina shule ya sekondari, wamejiwekea malengo ya kujenga vyumba 5 vya madarasa, ofisi 1 na nyumba ya mwalimu 1; Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020 utekelezaji wake ulikuwa kama ifuatavyo: - vyumba 3 vya madarasa vimekamilika mpaka hatua ya renta, Ofisi 1 na vyumba vitatu vya madarasa na nyumba ya mwalimu uko hatua ya boma/usawa wa madirisha, ufyatuaji wa matofali kwa ajili ya kazi ya ukamilishaji wa maboma umekamilika.

- Wananchi wa kata ya Bukandwe wamejiwekea malengo ya kujenga vyumba 4 vya madarasa katika shule ya sekondari Kanegere kwa nguvu zao ambapo hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020 ujenzi wa maboma 4 yalikuwa yamekamilika.

- Wananchi wa kata ya Ikunguigazi wamejiwekea malengo ya kujenga vyumba 2 vya madarasa, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020 ujenzi wa maboma 2 yalikuwa yamekamilika. Wananchi wa kata ya Nhomolwa wamejiwekea malengo ya kujenga chumba 1 cha darasa, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020 jengo lilikuwa hatua ya upauaji.



**Wananchi wa kata ya Masumbwe wakishiriki kuchimba misingi ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule ya sekondari Nyakasaluma**

#### (iii) Ujenzi wa nyumba za walimu

- Idadi ya nyumba za walimu wa shule za Sekondari imeongezeka kutoka nyumba 39 mwaka 2015 hadi nyumba 59 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 51.

- Kupitia fedha za Tanzania Education Authority (TEA), Halmashauri imefanikiwa kujenga nyumba ya walimu (Six in One) katika shule ya sekondari Nyasato.



**Muonekano wa nyumba ya walimu (Six in One) shule ya sekondari Nyasato**



**Muonekano wa nyumba ya walimu (Six in One) shule ya sekondari Iponya**

### (iv) Ujenzi wa Matundu ya vyoo

- Idadi ya matundu ya vyoo imeongezeka kutoka 124 mwaka 2015 hadi 178 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 100.

### (v) Idadi ya vyumba vya Maabara

- Idadi ya vyumba vya Maabara imeongezeka kutoka 37 mwaka 2015 hadi 48 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 29.

### (vi) Idadi ya viti na meza

- Idadi ya viti na meza imeongezeka kutoka 6,596 mwaka 2015 hadi 6,749 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 2.



**Mapokezi ya Viti na Meza kwa shule za sekondari kutoka Kampuni ya Uchimbaji wa Dhahabu Geita (GGM)**




**Mapokezi ya Viti na Meza Kwa shule za sekondari kutoka Benki ya CRDB**

### 3.1.1.2.2.4 UJENZI WA KIDATO CHA TANO NA SITA

Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe kwa sasa haina shule ya kidato cha tano na sita, hata hivyo katika kuboresha sekta ya elimu inatekeleza ujenzi wa miundombinu ya elimu ya kidato cha tano na sita katika shule ya sekondari ya Mbogwe, Lulembela na Nyakasaluma kwa kujenga mabweni, vyumba vya madarasa, vyoo na mabwalo ya chakula kwa wanafunzi. Ujenzi wa miundombinu katika shule ya sekondari Mbogwe na Lulembela uko katika hatua za ukamilishaji na ujenzi katika shule ya sekondari Nyakasaluma uko hatua za awali.

- Idadi ya Mabweni (Hosteli) imeongezeka kutoka 5 mwaka 2015 hadi 11 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 120.

- Kupitia fedha za Maombi Maalumu, Halmashauri imefanikiwa Kukamilisha ujenzi wa mabweni 3 na Bwalo 1 shule ya sekondari Mbogwe mbapo Jumla ya **Shilingi. 300,000,000** zilitumika kuwezesha shughuli hizo. Pia kupitia Fedha za EP4R Halmashauri imefanikiwa kujenga mabweni 2 katika shule ya sekondari Lulembela na mabweni 2 katika shule ya sekondari Mbogwe ambapo Jumla ya **Shilingi. 300,000,000** zilitumika kuwezesha shughuli hizo.



**Muonekano wa baadhi ya mabweni shule ya sekondari Mbogwe**




**Muonekano wa vyumba vya madarasa na ofisi shule ya sekondari Lulembela na Mbogwe**

### 3.1.1.3 AFYA NA USTAWI WA JAMII

**ILANI YA CHAMA CHA MAPINDUZI** ya mwaka 2015 Ibara ya 50 inasema, Kwa kuzingatia dhamira ya kuwa na wananchi wenye afya bora watakaoweza kushiriki katika shughuli mbalimbali za kiuchumi na kutoa huduma katika miaka mitano ijayo, Chama Cha Mapinduzi kitaielekeza Serikali kuendelea kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma bora za afya; Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe katika kutekeleza ibara hii imetekeleza kama ifuatavyo:

#### 3.1.1.3.1 UJENZI WA HOSPITALI YA WILAYA

Mwanzoni mwa mwezi Juni, 2020 Halmashauri imepokea fedha za ujenzi wa hospitali ya Wilaya kiasi cha shilingi. 500,000,000 ambapo ujenzi wake uko hatua ya kujenga msingi kama ambavyo jitihada za ujenzi huo zinavyoonekana kwenye picha hapo chini:




**Maandalizi ya kujenga OPD na Maabara Hospitali ya Wilaya ya Mbogwe**




**Mapokezi ya mbao PC 1400 (2*2) toka Kampuni ya Uchimbaji wa dhahabu Geita (GGM) kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Mbogwe**

### 3.1.1.3.2 UJENZI WA VITUO VYA AFYA NA ZAHANATI

- Vituo vya Afya vilivyopo ni 2, Idadi ya zahanati zimeongezeka kutoka 13 mwaka 2015 hadi 16 mwaka 2020; sawa na ongezeko la asilimia 23.

- Kupitia fedha za Uboreshaji wa vituo vya Afya, LGCDG na MMAM, Halmashauri imefanikiwa Kujenga wodi mbili, chumba cha kuhifadhia maiti, nyumba ya mganga na maabara katika vituo vya Iboya na Masumbwe na ujenzi umekamilika; Ujenzi hadi hatua ya ukamilishaji katika vituo vya afya vya Nhomolwa na Ikunguigazi, pia ujenzi wa zahanati katika vijiji vya Mpakali, Budoda na Mlange viko hatua ya ukamilishaji; Ambapo Jumla ya **Shilingi. 1,035,268,606** zilitumika kuwezesha shughuli za ujenzi wa vituo vya afya na zahanati.

- Kupitia Michango ya nguvu za wananchi, Wilaya imefanikiwa kuanza ujenzi wa **zahanati 69** zikiwa katika hatua mbalimbali za upauaji, lenta, maboma, madirisha, ukamilishaji na Misingi.



**Muonekano wa ujenzi wa kituo cha afya Ikunguigazi**




**Muonekano wa Maabara kituo cha afya Iboya**



**Muonekano wa nyumba ya kuhifadhi maiti kituo cha afya Iboya**




**Muonekano wa majengo ya kituo cha afya Masumbwe**



**UJENZI WA KITUO CHA AFYA NHOMOLWA**



**Meneja wa Kampuni ya GGM akikabidhi mkataba wa kutupatia vifaa vya thamani ya mil.100 kwa ajili ya kukamilisha zahanati 5 za Budoda, Shenda, Mpakali, Kagera na Kabanga.**

### 3.1.1.3.3 MAFANIKIO YA JUMLA SEKTA YA AFYA

- Idadi ya magari ya kubebea wagonjwa imeongezeka kutoka 1 maka 2015 hadi 3 mwaka 2020; sawa na ongazeko la asilimia 67.
- Idadi ya nyumba za watumishi wa afya imeongezeka kutoka 22 mwaka 2015 hadi 29 mwaka 2020; sawa na ongezeko la asilimia 32. Vilevile kuna nyumba 2 zilizo katika mbalimbali za ujenzi.
- Idadi ya watumishi wa afya imeongezeka kutoka 160 mwaka 2015 hadi 182 mwaka 2020; sawa na ongezeko la asilimia 14.
- Idadi ya vifo vya akinamama wajawazito imepungua kutoka 5 mwaka 2015 hadi 1 mwaka 2020; sawa na punguzo la 80 asilimia.

- Kasi ya maambukizi ya VVU/UKIMWI imeshuka kutoka wastani wa 3.8% mwaka 2015 na kufikia 2.9% mwaka 2020.

- Vituo vya kutolea huduma ya ushauri nasaha na kupima virusi vya UKIMWI imeongezeka kutoka vituo 12 mwaka 2015 hadi vituo 13 mwaka 2020.

- Mashirika yasiyokuwa ya kiserikali (NGO's) yanayosaidiana na Wilaya kupiga vita maambukizi mapya ya VVU yameongezeka na kufikia mwaka 2020 nayo ni Redcross, MDH, ICAP, SHIDEPHA na UMB.

- Kupitia ufadhili wa Mradi wa Kampeni ya Kitaifa ya Usafi na Mazingira, Halmashauri imefanikiwa Kuwezesha shughuli za Usafi wa Mazingira katika kata zote 17 kwa kujenga na kukarabati vyoo mashuleni na katika vituo vya kutolea huduma za afya ambapo Jumla ya **Shilingi.149,964,950** zilitumika kuwezesha shughuli hizo.

- Kupitia fedha za AGPAHI, BASKET FUND, CSSC, LISHE (IMMA), RBF, GLOBAL FUNDS, MDH, NTD, CHANJO (REC), SWASH (SWRSSP) na TACAIDS, Halmashauri imefanikiwa kuwezesha uboreshaji wa huduma za afya kwa wananchi wa Wilaya ya Mbogwe ambapo Jumla ya **Shilingi. 4,325,099,842** zilitumika kuwezesha shughuli hizo.

#### 3.1.1.3.4 DAWA, VIFAA TIBA NA VITENDANISHI

- Kwa kipindi cha mwaka 2015-2020 Halmashauri imefanikiwa kupokea na kutumia kiasi cha **Shilingi. 613,252,206** kwa ajili ya kununua dawa, vifaa tiba na vitendanishi ili kuboresha huduma za afya kwa wananchi wa Wilaya ya Mbogwe. Hali ya upatikanaji wa dawa mhimu imeongezeka kutoka asilimia 65 mwaka 2015 hadi asilimia 79.3

### 3.1.1.4 UJENZI WA STENDI YA MABASI

- Kupitia fedha za mapato ya ndani, Halmashauri imefanikiwa kuanza ujenzi wa stendi ya mabasi Masumbwe - Mzambarauni ili kuongeza mapato ya ndani ya Halmashauri na utekelezaji wake uko katika hatua ya ukamilishaji wa majengo (Nyumba ya wasafiri, Nyumba ya Mlinzi, Ofisi, choo, matengenezo ya barabara na uwekaji wa kalvati) ambapo kiasi cha **Shilingi. 41,000,000** zimetumika.



**Muonekano wa ujenzi wa stendi ya mabasi katika Mji wa Masumbwe**

### 3.1.2 HUDUMA ZA KIUCHUMI

Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe imeendelea kuishirikisha jamii katika shughuli za uzalishajimali hususani kupitia kilimo, uvuvi na ufugaji ili kuimarisha kipato cha kaya na cha mtu mmoja mmoja, kutoa ajira kwa wananchi wakiwemo akina mama na vijana.

#### 3.1.2.1 KILIMO, UMWAGILIAJI NA USHIRIKA

Wilaya inakadiriwa kuwa na eneo linalofaa kwa kilimo ambalo ni Hekta 198,997. Takribani asilimia 79% ya wakazi wa Wilaya ya Mbogwe wanajishughulisha na kilimo. Kwahiyo sekta ya kilimo ndiyo uti wa mgongo wa uchumi kwa wakazi wa Wilaya ya Mbogwe ambao wanajishughulisha na kilimo cha mazao mbalimbali yakiwemo mazao ya chakula na mazao ya biashara.

**ILANI YA CHAMA CHA MAPINDUZI** ya mwaka 2015 Ibara ya 22 inaelekeza, Katika kipindi cha mwaka 2015 - 2020, Chama Cha Mapinduzi kitaielekeza Serikali kutilia mkazo utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Programu ya Kuendeleza Kilimo (Agricultural Sector Development Programme – ASDP II) pamoja na miradi ya Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa (BRN) ili kufikia malengo makuu ya kukifanya kilimo kuwa cha kisasa na cha kibiashara. Kufuatia maelekezo hayo Halmashauri ya Wilaya imepata mafanikio kama ifuatavyo:

- Upatikanaji wa zana za kilimo (Matrekta makubwa) umeongezeka kutoka matrekta 12 maka 2015 hadi matrekta 21 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 75.
- Upatikanaji wa zana za kilimo (Matrekta madogo) umeongezeka kutoka matrekta 26 mwaka 2015 hadi matrekta 32 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 25.
- Upatikanaji wa zana za kilimo (Majembe ya kukokotwa na wanyamakazi) imeongezeka kutoka majembe 4,313 mwaka 2015 hadi majembe 4,517 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 4.7.
- Usambazaji wa mbolea umeongezeka kutoka tani 19,826 mwaka 2015 hadi tani 22,684 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 14.4.
- Matumizi ya mbolea ya samadi na mboji yameongezeka kutoka tani 4,959 mwaka 2015 hadi tani 5023 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 3.3.
- Matumizi ya mbolea za viwandani yameongezeka kutoka tani 14870 mwaka 2015 hadi tani 15844 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 6.9.
- Usambazaji wa mbegu bora za mazao ya chakula umeongezeka kutoka tani 1983 mwaka 2015 hadi tani 2561 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 30.2.
- Usambazaji wa mbegu za mazao ya biashara umeongezeka kutoka tani 400 mwaka 2015 hadi tani 496 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 28.

- Idadi ya wakulima waliopata mafunzo ya kanuni bora za kilimo imeongezeka kutoka 5,250 mwaka 2015 hadi 7,677 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 46.2
- Idadi ya mashamba darasa imeongezeka kutoka 287 mwaka 2015 hadi 359 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 25.
- Ongezeko la uzalishaji wa mazao ya kipaumbele ya chakula umeongezeka kutoka tani 244,400 mwaka 2015 hadi tani 329192 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 34.7
- Halmashauri imetumia kiasi cha **shilingi. 2,800,000** kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa kitalu nyumba kilichopo kijiji cha Bulugala katika kata ya Nyasato.



**Muonekano wa Teknolojia ya Kitalu nyumba kuwakomboa vijana kiuchumi (Greenhouse) kijiji Cha Bulugala**



**Usambazaji wa Matrekta kwa Mkopo kupitia Benki ya Kilimo**

### 3.1.2.2 MIFUGO NA UVUVI

**ILANI YA CHAMA CHA MAPINDUZI** ya mwaka 2015 Ibara ya 25 inaelekeza, Katika kipindi cha Ilani hii ya 2015-2020, Chama Cha Mapinduzi kitaielekeza Serikali yake kuiendeleza Sekta ya Mifugo. Kufuatia maelekezo hayo Halmashauri ya Wilaya imepata mafanikio kama ifuatavyo:

i. Idadi ya malambo ya kunyweshea mifugo imeongezeka kutoka 23 mwaka 2015 hadi 41 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 78.

ii. Idadi ya wafugaji bora imeongezeka kutoka 40 mwaka 2015 hadi 65 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 62.

iii. Idadi ya vikundi vya wafugaji bora imeongezeka kutoka vikundi 4 mwaka 2015 hadi 6 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 50.

iv. Idadi ya wafugaji waliopata mafunzo ya ufugaji bora imeongezeka kutoka 420 mwaka 2015 hadi 1,013 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 141.

v. Idadi ya ng'ombe wa kisasa imeongezeka kutoka 60 mwaka 2015 hadi 81 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 35.

vi. Kupitia ufadhili wa Mradi wa Agricultural Sector Development Plans (ASDP) Halmashauri imenunua Mashine ya kutotolesha vifaranga, Majogoo 120 na Mitetea 80 kwa ajili ya kuboresha ufugaji wa kuku wa asili katika vijiji vya Ilangale, Nyakasaluma, Shinyanga B, Bulugala, Ilolangulu, Ibambula na Nambubi na mawe 3 ya kuchinjia katika Kata za Lulembela, Lugunga na Mbogwe yamejengwa, ambapo Jumla ya **Shilingi. 11,662,980** zilitumika kukamilisha miradi hiyo.

- Kwa kipindi cha mwaka 2015-2020 Halmashauri imetumia kiasi cha **Shilingi. 8,000,000** kwa ajili ya ununuzi wa chanjo za mifugo na kufanikiwa kuchanja ng'ombe 16,000. Halmashauri iligawa dawa za ruzuku za kuogeshea mifugo kiasi cha lita 73.5 katika kata za Nyasato, Mbogwe na Lugunga, ambapo idadi ya mifugo walioogeshwa ni ng'ombe 24,000, mbuzi 11,000 na kondoo 3,000. Halmashauri imetumia kiasi cha **Shilingi. 12,500,000** kujenga ofisi na choo cha kisasa katika mnada wa mifugo uliopo katika kijiji cha Masumbwe.

### 3.1.2.3 ARDHI NA MALIASILI

**ILANI YA CHAMA CHA MAPINDUZI ya Mwaka 2015 Ibara ya 31 (b**) inaeleza kutatua migogoro ya mipaka kati ya wananchi na maeneo ya jirani na hifadhi kwa kushirikisha wadau katika kuhakiki mipaka ya maeneo ya hifadhi kwa kuweka alama za kudumu; kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi; na kuzingatia utawala wa Sheria katika kusimamia rasilimali za maliasili; Kufuatia mkakati huo Halmashauri ya Wilaya imepata mafanikio yafuatayo:


- Idadi ya mashamba yaliyopimwa imeongezeka kutoka 120 mwaka 2015 hadi 316 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 163.
- Idadi ya viwanja vya makazi vilivyopimwa imeongezeka kutoka 963 mwaka 2015 hadi 2,149 sawa na ongezeko la asilimia 123.
- Ukuzaji na upandaji miti umeongezeka kutoka miti 299,434 mwaka 2015 hadi miti 1,519,991 sawa na ongezeko la asilimia 407.
- Halmashauri imefanikiwa kununua Mashine au kifaa cha kupimia viwanja (Total Station) kupitia fedha za Mfuko wa Jimbo ambapo kiasi cha **Shilingi. 23,611,000** zilitumika na zoezi la upimaji wa viwanja linaendelea katika kata 17 zilizopo katika Wilaya ya Mbogwe.
- Halmashauri imefanikiwa kupima Viwanja 2,994 kwa ajili ya matumizi ya makazi, biashara na taasisi.
- Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi ya vijiji Kumi na Saba (17) umeandaliwa na kukamilika.
- Maeneo yenye ukubwa wa hekta 211.06 yametengwa katika vijiji vya Bukandwe (HA. 133.20), Lubeho (HA. 61.24), Mkombozi (HA. 2.20), Kibondo A (HA. 0.81) na Lugito (HA. 13.61) kwa shughuli za viwanda.



**Mashine ya kupimia viwanja iliyonunuliwa kupitia fedha za Mfuko wa Jimbo**



**MWENYEKITI WA KIJIJI CHA MLALE AKIMKABIDHI HATI YA KIMILA MMOJA WA WANANCHI WA KIJIJI HICHO**




**RAMANI YA MPANGO KINA WA MATUMIZI YA ARDHI YA ENEO LA MAKAZI KIJIJI CHA MLALE**

### 3.1.3 UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

#### 3.1.3.1 MAENDELEO YA JAMII

**ILANI YA CHAMA CHA MAPINDUZI** ya mwaka 2015 Ibara ya 164, 165, 166, 168, 170 na 172 inaelekeza na kuhimiza kuendeleza Makundi Maalumu, na ushirikishwaji wa wananchi katika shughuli za Maendeleo na kuyaendeleza makundi mbalimbali katika Jamii. Kufuatia maelekezo hayo Halmashauri ya Wilaya imepata mafanikio kama ifuatavyo:

- Kwa kipindi cha mwaka 2015-2020 Halmashauri imefanikiwa kutoa mikopo kwenye vikundi vya ujasiriamali yenye thamani ya **Shilingi. 93,827,000** ambapo vikundi 45 vya wanawake, vikundi 24 vya vijana na vikundi 7 vya watu wenye ulemavu vyote hivi vimepatiwa mikopo vilivyopo katika kata 17 za Wilaya ya Mbogwe vinavyojishughulisha na Biashara ndogondogo kama vile mama lishe, uuzaji dagaa, Kilimo, Ufugaji, Useremala na ushonaji.




**Muonekano wa shughuli za uzalishaji mali kwa akina mama na vijana katika Wilaya ya Mbogwe**

### 3.1.3.2 MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII (TASAF)

Tangu kuanzishwa kwa Mpango wa TASAF awamu ya tatu (Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini) mwaka 2015, Wilaya ya Mbogwe ina jumla ya wanufaika 4309, wanufaika hawa wameweza kuanzisha miradi midogo midogo kama vile ufugaji, ufundi cherehani ili kujiongezea kipato na kuinua uchumi ngazi ya kaya na wengine wameweza kuboresha makazi.

**ILANI YA CHAMA CHA MAPINDUZI** ya mwaka 2015 Ibara ya 70 (c) inaelekeza Kuimarisha Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) ili kukamilisha Utekelezaji wa Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini (TASAF III) na kubuni programu nyingine za kusaidia jamii kupambana na umasikini; Kufuatia maelekezo hayo Halmashauri ya Wilaya imepata mafanikio kama ifuatavyo:

- Kwa kipindi cha mwaka 2015-2020 Halmashauri imepokea fedha kiasi cha **Shilingi. 6,913,338,950** kwa ajili ya kufanikisha shughuli za Uhawilishaji wa fedha ikihusisha fedha za ruzuku ya msingi (chakula, maladhi na tiba) na ruzuku ya masharti (kupeleka watoto klinik na shuleni). Aidha kwa kuzingatia masharti hayo, walengwa wa TASAF wameweza kuboresha maisha yao kwa kuhakikisha watoto wao wanapelekwa kliniki na shuleni. Shughuli hizi za uhawilishaji fedha zimeleta mafanikio makubwa kwa walengwa wa TASAF.






**Muonekano wa miradi mbalimbali ya walengwa WA TASAF Katika Wilaya Mbogwe**

### 3.1.3.3 MWENENDO WA MAKUSANYO YA FEDHA ZA MAPATO YA NDANI NA RUZUKU YA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA MWAKA 2015 HADI MWEZI MEI, 2020

**ILANI YA CHAMA CHA MAPINDUZI** Ibara ya 148 (c) na (d) ya mwaka 2015 inasema Ili kuziendeleza Mamlaka za Serikali za Mitaa, katika kipindi cha 2015- 2020 ya Utekelezaji wa Ilani hii, CCM itahakikisha kwamba, Serikali inatekeleza yafuatazo:- Kuendelea kuongeza kiwango cha ruzuku kutoka Serikali Kuu kinachopelekwa kwenye Halmashauri zote nchini kupitia Bajeti ya Serikali ya kila mwaka kwa kadri ya uchumi utakavyokua; Kuendelea kuzihamasisha Halmashauri zote nchini kubuni vyanzo vipya vya mapato ya ndani (own sources) pamoja na kuimarisha mifumo ya ukusanyaji na udhibiti wa mapato; Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe katika kutekeleza ibara hii imetekeleza kama ifuatavyo:

#### (a) MHUTASARI WA MAKUSANYO YA FEDHA ZA MAPATO YA NDANI KUANZIA 2015 HADI MWEZI MEI, 2020

| S/N | MWAKA WA FEDHA | MAKISIO | MAPATO HALISI | % |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 2015/2016 | 257,341,440 | 172,036,049 | 67 |
| 2. | 2016/2017 | 1,064,893,000 | 715,099,089 | 67 |
| 3. | 2017/2018 | 1,199,120,000 | 685,780,723 | 57 |
| 4. | 2018/2019 | 1,207,134,000 | 628,910,843 | 52 |
| 5. | 2019/2020 | 906,684,000 | 919,029,762 | 101 |
| **JUMLA** | | **4,635,172,440** | **3,120,856,466** | **67** |

#### (b) MHUTASARI WA MAPATO MIRADI YA MAENDELEO KISEKTA KUANZIA 2015 HADI MWEZI MEI, 2020

| S/N | MWAKA | FEDHA TOLEWA | SEKTA ZILIZOPOKEA FEDHA | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 2015/16 | 4,402,228,016 | (i) | Mifugo | 11,662,980 |
| | | | (ii) | Afya | 576,345,430 |
| | | | (iii) | Dawa, Vifaa tiba na Vitendanishi | 100,931,480 |
| | | | (iv) | Maji | 287,532,694 |
| | | | (v) | Elimu Sekondari | 588,567,265 |
| | | | (vi) | Elimu bila Malipo – Msingi | 318,229,438 |
| | | | (vii) | Elimu bila Malipo – Sekondari | 116,155,999 |
| | | | (viii) | Utawala (HQ, Nyumba & CDCF) | 645,196,000 |
| | | | (ix) | Barabara (Roadfund) | 697,771,230 |
| | | | (x) | TASAF | 1,059,835,500 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 2. | 2016/17 | 5,073,200,756 | (i) | Barabara (Roadfund) | 1,046,843,618 |
| | | | (ii) | Maji | 105,954,223 |
| | | | (iii) | Elimu bila Malipo – Msingi | 377,366,648 |
| | | | (iv) | Elimu bila Malipo – Sekondari | 208,428,000 |
| | | | (v) | Afya | 593,115,000 |
| | | | (vi) | Dawa, Vifaa tiba na Vitendanishi | 151,883,975 |
| | | | (vii) | Utawala (HQ, CDCF & LGCDG) | 1,031,483,000 |
| | | | (viii) | TASAF | 1,558,126,292 |
| 3. | 2017/18 | 4,679,863,912 | (i) | Afya | 1,696,985,423 |
| | | | (ii) | Dawa, Vifaa tiba na Vitendanishi | 130,915,856 |
| | | | (iii) | Elimu bila Malipo – Msingi | 398,410,344 |
| | | | (iv) | Elimu bila Malipo – Sekondari | 191,662,498 |
| | | | (v) | Utawala (CDCF) | 44,920,000 |
| | | | (vi) | Elimu Sekondari | 260,491,410 |
| | | | (vii) | Elimu Msingi | 195,200,000 |
| | | | (viii) | Maji | 79,954,223 |
| | | | (ix) | TASAF | 1,681,324,158 |
| 4. | 2018/19 | 4,595,901,536 | (i) | Maji | 265,016,834 |
| | | | (ii) | Dawa, Vifaa tiba na Vitendanishi | 149,758,668 |
| | | | (iii) | Elimu bila Malipo – Msingi | 417,800,000 |
| | | | (iv) | Elimu bila Malipo – Sekondari | 201,933,171 |
| | | | (v) | Afya | 1,464,333,863 |
| | | | (vi) | Utawala (CDCF) | 44,444,000 |
| | | | (vii) | Elimu Sekondari | 1,024,100,000 |
| | | | (viii) | Elimu Msingi | 100,000,000 |
| | | | (ix) | TASAF | 928,515,000 |
| 5. | 2019/20 | 4,452,928,522 | (i) | Dawa, Vifaa tiba na Vitendanishi | 79,762,227 |
| | | | (ii) | Afya | 1,168,599,743 |
| | | | (iii) | Ujenzi wa Hospitali | 500,000,000 |
| | | | (iv) | Elimu bila Malipo – Msingi | 579,850,356 |
| | | | (v) | Elimu bila Malipo – Sekondari | 222,631,398 |
| | | | (vi) | Utawala (HQ & CDCF) | 141,546,798 |
| | | | (vii) | Elimu Msingi | 75,000,000 |
| | | | (viii) | TASAF | 1,685,538,000 |
| **JUMLA** | | **23,254,122,842** | | | **23,254,122,842** |

## 3.2 IDARA NA TAASISI ZINGINE ZA SERIKALI

### 3.2.1 TANESCO

**ILANI YA CHAMA CHA MAPINDUZI** ya mwaka 2015 Ibara ya 43 inasema, Chama Cha Mapinduzi kitaielekeza Serikali kuongeza kwa kiwango kikubwa uzalishaji wa nishati ili kuendelea kukuza Sekta hiyo na kuongeza mchango wake kwenye Pato la Taifa; Wilaya ya Mbogwe katika kutekeleza ibara hii imetekeleza kama ifuatavyo:

Kwa kipindi cha mwaka 2015-2020 Serikali kupitia Mpango wa Usambazaji Umeme Vijijini (REA) imetekeleza miradi ya ujenzi wa Umeme katika wilaya ya Mbogwe, ambapo miradi hii imegawanyika katika vipindi tofauti kama ifuatavyo:

- Awamu ya kwanza, Mradi ulitekelezwa na **ELECTRICITY V** huu ndio mradi uliofika kwa mara ya kwanza katika Wilaya ya Mbogwe ukizinduliwa na Waziri wa Nishati na Madini wa kipichi hicho Mh. George Simbachawene mnamo **18.09.2013.** Mradi huu ulifadhiliwa kwa mkopo wa Benki ya Maendeleo ya Africa (ADB) ambao ulitekelezwa kwa awamu mbili tofauti.

  **Kampuni ya ELTEL AB.** Kampuni hii kutoka Nchini Sweden ilifanikiwa kujenga jumla ya Transifoma kumi na saba (17) katika vijiji vifuatavyo: Ushirika, Mlale, Bwelwa, Nanda, Lubeho, Ilangale, Nyakafulu, Kakumbi na Lugunga. Aidha pia baadhi ya vitongoji vya Masumbwe vikiwemo Mzambarauni, Kagri, Mang'ombe, Kona Nne, Stendi, Mashineni vilipata umeme katika awamu ya kwanza ya mradi huu. Mradi huu umekamilika kwa asilimia 100.

- Awamu ya pili, Mradi ulitekelezwa na Shirika la Umeme Tanzania (**TANESCO**) ambapo jumla ya Transfoma Tano (5) ziliongezwa. Aidha, vijiji na vitongoji vilinufaika tena kwa awamu hii ya pili. Maeneo yaliyonufaika ni Iboya na vitongoji vya Iloganzala, Kagri, Shinyanga 'B', Nyerere na katikati ya mji wa Masumbwe na hivyo kufanya jumla ya transfoma ishirini na mbili (22) katika mradi huu. Mradi huu umekamilika kwa asilimia mia moja 100.

- Awamu ya tatu, Mradi wa REA II ulitekelezwa na mkandarasi **M/S NAKUROI INVESTMENTS LIMITED** na ulikamilika mnamo mwezi Desemba 2017. Vijiji vilivyonufaika na mradi huu ni pamoja na Bwendamwizo na Ngemo vilivyopo katika Kata ya Ngemo, Nambubi kilichopo Kata ya Mbogwe, Ilolangulu katika Kata ya Ilolangulu, Isebya katika Kata ya Isebya, Lulembela na kashelo katika Kata ya Lulembela, Bugalagala katika Kata ya Ikobe, Ikunguigazi katika Kata ya Ikunguigazi. Vingine ni Bukandwe na Kanegere katika Kata ya Bukandwe, Ng'homolwa katika Kata ya Ng'homolwa, Shenda katika kata ya Masumbwe pamoja na Iponya katika Kata ya Iponya. Jumla ya transfoma ishirini na mbili (22) ziliwashwa. Mradi huu umekamilika kwa asilimia 100.

- Awamu ya Nne, Mradi wa REA III Awamu ya Kwanza. Mradi huu umekwishaanza na unatekelezwa na Mkandarasi M/S WHITE CITY /GUANGDOUNG J.V. Vijiji 33 vinanufaika na mradi huu, vijiji hivyo ni pamoja na Nyakasaluma, Budoda, Ilangale, Msendamila, Mubamba, Nyang'holongo, Muungano, Ishingamva, Kanegere Nyashimba, Kashelo, Bugomba, Mtakuja, Nyakonga, Ibambula, Kabanga, Kasaka, Bulugala, Nyasato, Mlange, Bulilila, Mgaya, Nsango, Kasosobe, Shinyanga A, Shinyanga B, Shinyanga B Sekondari, Ikobe, Busabaga, Kagera, Mwigiro, Buzigozigo na Kanangwe. Ambapo hadi sasa mkandarasi yupo site kwa ajili ya utekelezaji.

- Katika kutekeleza kaulimbiu ya serikali wilaya imefanikiwa kupeleka umeme katika eneo la wachimbaji wadogo **Nyakafuru** na kusambaza umeme katika **Makalasha**, **mialo na vibanda vya biashara**. Pia kwa sasa umeme unapelekwa kwenye Kiwanda cha SHIRECU 1984 maeneo ya Kagri. Sambamba na hilo wilaya imeweza kupeleka umeme kwenye pampu za maji zikiwemo katika kijiji cha Shenda pampu ya maji na Nyakafuru pampu ya maji ambazo zimekamilika kwa asilimia 100.



**TRANSFOMA HII INAHUDUMIA WATEJA WADOGO WADOGO WA MASHINE ZA KUKOBOA MPUNGA (KIBONDO A)**



**TRANSFOMA HII YA PAMPU YA MAJI NYAKAFURU**

### 3.2.2 WAKALA WA BARABARA VIJIJINI NA MIJINI (TARURA)

Ibara ya 39 ya ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 inasema, Katika kipindi cha mwaka 2015 hadi 2020, Chama Cha Mapinduzi kitaielekeza Serikali kuendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa barabara na madaraja, vivuko, nyumba na majengo ya Serikali kwa lengo la kuongeza kasi ya maendeleo ya kiuchumi na huduma za kijamii. Wilaya ya Mbogwe katika kutekeleza ibara hii imetekeleza kama ifuatavyo: Wilaya ya Mbogwe ina mtandao wa barabara wenye urefu wa kilomita 1,321.62 (sawa na ongezeko la 57%), mpaka kufikia mwaka 2020 jumla ya km 427 (sawa na ongezeko la 29%) za barabara zilikuwa zimefanyiwa matengenezo na jumla ya midomo 154 (sawa na ongezeko la 56%) ya kalavati imejengwa. Mchanganuo wa mtandao wa barabara zilizojengwa zimeorozeshwa hapo chini:

**A: MATENGENEZO YA KAWAIDA**

i. Nambubi - Kanangwe – Nyashinge km 12.5
ii. Nyashinge – Isebya km 6
iii. Mwingiro - Mgerere – Isebya km 6.5
iv. Ikunguigazi - Mwingiro km 14.9
v. Nyakafulu town roads km 13.8
vi. Masumbwe town roads km 9.2
vii. KanegereMbugani – Maguta km 3
viii. Maguta - Nyanhwiga - Kahama border km 3
ix. Masumbwe – Ilangale km 3
x. Bugalagala – Kiseke km 2
xi. Lulembela – Ibambula km 2
xii. Lulembela – Mtakuja km 6
xiii. Kagera - Buzigozigo–Bugalagala km 7.5
xiv. Bunyihuna - Busambilo – Nsango km 11.5
xv. Ilangale - Shinyanga – Bugelenga km 16
xvi. Iponya - Bunyihuna km 4
xvii. Iponya - Nyashimba- Kahama border km 10.6
xviii. Lubeho – Ikalanga km 7
xix. Iponya – Buluhe km 3
xx. Kisumo – Ilolangulu km 12.9
xxi. Ilolangulu - Nyanhwale – Nanda km 8
xxii. Ivumwa - Ushirika – Shibutwe km 6
xxiii. Lugunga – Mponda km 6

xxiv. Bulugala – Isungabula km 3
xxv. Mbogwe Dc Town roads km 3
xxvi. Bwelwa- Mlale km 3
xxvii. Bulugala - Kasaka – Bwelwa km 8
xxviii. Mlange -Shibutwe km 2
xxix. Bwendamwizo – Ngemo km 5
xxx. Ushirika - Buzigula - Geita Border km 8.7
xxxi. Bulugala - Bulilila – Mlange km 9
xxxii. Nyasato – Ushirika km 5
xxxiii. Nyang'holongo - Kisumo – Nanda km 10
xxxiv. Mkweni - Nyanhwiga - Ngh'omolwa km 14
xxxv. Kanegere Prison – Nhungwiza km 12.5
xxxvi. Lugunga – Nhungwiza km 13
xxxvii. Lulembela – Kiseke km 12
xxxviii. Masumbwe – Nsango km 27
xxxix. Mlange -Shibutwe km 10
xl. Kagera -Mwamitilwa - Ikunguigazi km 6
xli. Butengu - Ikobe - Bukombe border km 10
xlii. Mzambarauni – Budoda km 10
xliii. Shenda – Mwabomba km 4.5
xliv. Busafya - Nyakasaluma - Kanegere Prison km 10
xlv. Bwendaseko – Ivumwa km 8
xlvi. Isebya - Nyashinge – Lwamgasa km 4
xlvii. Ushirika - Kadoke – Ntono km 5.5
xlviii. Ilolangulu - Kisumo - Bukombe Border km 18.8
xlix. Shenda - Mwabomba - Kahama Border km 3
l. Bwelwa - Nanda - Bukombe Border km 4
li. Lugunga - Mpakali – Nhungwiza km 13.6
lii. Kiseke - Isebya – Ilolangulu km 10

**B: MATENGENEZO YA SEHEMU KOROFI**

i. Nambubi - Kanangwe – Nyashinge km 1.7
ii. Nyashinge – Isebya km2
iii. Mwingiro - Mgerere – Isebya km 1
iv. KanegereMbugani – Maguta km 1.5
v. Maguta - Nyanhwiga - Kahama border km 3
vi. Masumbwe – Ilangale km 1
vii. Bugalagala – Kiseke km 1.5
viii. Lulembela – Ibambula km 1.5
ix. Kagera - Buzigozigo – Bugalagala km 5

x. Bunyihuna - Busambilo – Nsango km 1.7
xi. Ilangale - Shinyanga – Bugelenga km 2.5
xii. Iponya - Bunyihuna km 1
xiii. Iponya - Nyashimba- Kahama border km 1.5
xiv. Lubeho – Ikalanga km0.5
xv. Iponya – Buluhe km 1
xvi. Kisumo – Ilolangulu km 1.7
xvii. Ilolangulu - Nyanhwale – Nanda km 1.5
xviii. Ivumwa - Ushirika – Shibutwe km 1
xix. Lugunga – Mponda km 3
xx. Bulugala – Isungabula km 1.5
xxi. Bwelwa- Mlale km 0.2
xxii. Bulugala - Kasaka – Bwelwa km 0.5
xxiii. Mlange -Shibutwe km 0.5
xxiv. Bwendamwizo – Ngemo km 0.5
xxv. Ushirika - Buzigula - Geita Border km 0.7
xxvi. Nyang'holongo - Kisumo – Nanda km 0.5
xxvii. Mkweni - Nyanhwiga - Ngh'omolwa km 0.5
xxviii. Kanegere Prison – Nhungwiza km 0.5
xxix. Lugunga – Nhungwiza km 0.5
xxx. Lulembela – Kiseke km 0.5
xxxi. Masumbwe – Nsango km 1.5
xxxii. Butengu - Ikobe - Bukombe border km 0.5
xxxiii. Mzambarauni – Budoda km 0.2
xxxiv. Isebya - Nyashinge – Lwamgasa km 0.5
xxxv. Shenda - Mwabomba - Kahama Border km 0.5
xxxvi. Bwelwa - Nanda - Bukombe Border km 0.5
xxxvii. Lugunga - Mpakali – Nhungwiza km 1
xxxviii. Kiseke - Isebya – Ilolangulu km 1
xxxix. Ikunguigazi – Mwingilo km 0.5

**C: MATENGENEZO YA MUDA MAALUM**

i. Nambubi - Kanangwe – Nyashinge km 2.5
ii. Nyashinge – Isebya km 1
iii. Ikunguigazi - Mwingiro km 2
iv. Nyakafulu town roads km 6.9
v. Masumbwe town roads km 4.9
vi. Kagera - Buzigozigo – Bugalagala km 0.5
vii. Bunyihuna - Busambilo – Nsango km 0.5
viii. Ilangale - Shinyanga – Bugelenga km1

ix. Iponya - Nyashimba- Kahama border km 1.5
x. Lubeho – Ikalanga km 1
xi. Iponya – Buluhe km 1
xii. Kisumo – Ilolangulu km 1
xiii. Ilolangulu - Nyanhwale – Nanda km 2
xiv. Ivumwa - Ushirika – Shibutwe km 1.5
xv. Lugunga – Mponda km 2
xvi. Bulugala - Kasaka – Bwelwa km 1
xvii. Mlange -Shibutwe km 2
xviii. Ushirika - Buzigula - Geita Border km 1
xix. Bulugala - Bulilila – Mlange km 2.5
xx. Nyasato – Ushirika km 1.5
xxi. Nyang'holongo - Kisumo – Nanda km 2.5
xxii. Mkweni - Nyanhwiga - Ngh'omolwa km 1.5
xxiii. Lulembela – Kiseke km 1
xxiv. Masumbwe – Nsango km 4
xxv. Butengu - Ikobe - Bukombe border km 0.5
xxvi. Mzambarauni – Budoda km 0.5
xxvii. Shenda – Mwabomba km 2
xxviii. Busafya - Nyakasaluma - Kanegere Prison km 4.5
xxix. Ushirika - Kadoke – Ntono km 5
xxx. Ilolangulu - Kisumo - Bukombe Border km 12.5
xxxi. Shenda - Mwabomba - Kahama Border km 1
xxxii. Bwelwa - Nanda - Bukombe Border km 1
xxxiii. Lugunga - Mpakali – Nhungwiza km 3
xxxiv. Kiseke - Isebya – Ilolangulu km 5.5

**D: UJENZI WA MAKALVATI (Midomo)**

i. Nambubi - Kanangwe – Nyashinge (midomo 2)
ii. Nyashinge – Isebya km (midomo 4)
iii. Mwingiro - Mgerere – Isebya (midomo 4)
iv. Ikunguigazi – Mwingiro (midomo 3)
v. KanegereMbugani – Maguta (midomo 2)
vi. Maguta - Nyanhwiga - Kahama border (midomo 1)
vii. Masumbwe – Ilangale (midomo 1)
viii. Bugalagala – Kiseke (midomo 1)
ix. Lulembela – Ibambula (midomo 1)
x. Lulembela – Mtakuja (midomo 1)
xi. Kagera - Buzigozigo – Bugalagala (midomo 1)
xii. Bunyihuna - Busambilo – Nsango (midomo 4)

xiii. Ilangale - Shinyanga – Bugelenga (midomo 5)
xiv. Iponya – Bunyihuna (midomo 1)
xv. Iponya - Nyashimba- Kahama border (midomo 5)
xvi. Lubeho – Ikalanga (midomo 1)
xvii. Iponya – Buluhe (midomo 2)
xviii. Kisumo – Ilolangulu (midomo 4)
xix. Ilolangulu - Nyanhwale – Nanda (midomo 6)
xx. Ivumwa - Ushirika – Shibutwe (midomo 2)
xxi. Lugunga – Mponda (midomo 2)
xxii. Bulugala - Kasaka – Bwelwa (midomo 7)
xxiii. Mlange –Shibutwe (midomo 7)
xxiv. Bwendamwizo – Ngemo (midomo 3)
xxv. Ushirika - Buzigula - Geita Border (midomo4)
xxvi. Bulugala - Bulilila – Mlange (midomo 4)
xxvii. Nyang'holongo - Kisumo – Nanda (midomo 4)
xxviii. Mkweni - Nyanhwiga - Ngh'omolwa (midomo 6)
xxix. Kanegere Prison – Nhungwiza (midomo 4)
xxx. Lugunga – Nhungwiza (midomo 4)
xxxi. Lulembela – Kiseke (midomo 2)
xxxii. Masumbwe – Nsango (midomo 7)
xxxiii. Kagera -Mwamitilwa – Ikunguigazi (midomo 3)
xxxiv. Butengu - Ikobe - Bukombe border (midomo 1)
xxxv. Mzambarauni – Budoda (midomo 1)
xxxvi. Shenda – Mwabomba (midomo 1)
xxxvii. Busafya - Nyakasaluma - Kanegere Prison (midomo 8)
xxxviii. Bwendaseko – Ivumwa (midomo 2)
xxxix. Isebya - Nyashinge – Lwamgasa (midomo 1)
xl. Ushirika - Kadoke – Ntono midomo 6
xli. Ilolangulu - Kisumo - Bukombe Border (midomo 9)
xlii. Shenda - Mwabomba - Kahama Border (midomo3)
xliii. Bwelwa - Nanda - Bukombe Border (midomo1)
xliv. Lulembela – Bugomba – Bukombe border (midomo3)
xlv. Lugunga - Mpakali – Nhungwiza (midomo2)
xlvi. Mkweni – Ibondo – Kanegere-Mlimani (midomo5)
xlvii. Lulembela –kiseke (Boksi kalvati1)
xlviii. Kiseke - Isebya – Ilolangulu (Midomo2)



**UJENZI WA BARABARA MPYA YA USHIRIKA – KADOKE – NTONO (KM 5.5) INAONESHA KABLA YA UTEKELEZAJI NA BAADA YA UTEKELEZAJI**



**UJENZI WA BARABARA YA ILOLANGULU – KISUMO – BUKOMBE BORDER (KM 16.3) INAONESHA KABLA YA UTEKELEAJI NA BAADA YA UTEKELEZAJI**



**UJENZI WA MAKALVATI BARABARA YA LUGUNGA – NHUNGWIZA – KANEGERE PRISON (MIDOMO 3) KABLA YA UTEKELEZAJI NA BAADA YA UTEKELEZAJI**

### 3.2.3 WAKALA WA HUDUMA ZA MISITU TANZANIA (TFS)

Ibara ya 39 ya ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 inasema, Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Serikali itaendelea kuchukua hatua za kuhakikisha kwamba Sekta ya Maliasili inazidi kuimarika ili kuyafanya mazao yatokanayo na maliasili hususan misitu na nyuki yanaendelea kuchangia katika ukuaji wa uchumi, kuwaongezea wananchi kipato na kuongeza fursa za ajira. Wilaya ya Mbogwe katika kutekeleza ibara hii imetekeleza kama ifuatavyo:

Kwa kipindi cha Miaka Mitano (**2015-2020**), Shughuli zifuatazo zimetekelezwa kwa Ushirikiano wa Halmashauri ya Wilaya na Ofisi ya Mhifadhi Misitu Wilaya (DFC) kama ilivyokuwa katika Ilani ya chama cha Mapinduzi kama ifuatavyo:

**i. Zoezi la Utunzaji Mazingira,Vyanzo vya Maji na Zoezi la Upandaji Miti Kitaifa**

TFS imeendelea Kufanya Doria Maeneo mbalimbali ya Misitu ya Mkweni na Maeneo ya Wazi ili kukabiliana na ukataji holela wa miti na uchomaji Mkaa kama sehemu ya utunzaji mazingira. Jumla ya Miti/Miche 1,519,991 ilizalishwa na kupandwa maeneo mbalimbali ya Wilaya kwa kutoa elimu kwa Watu binafsi, Vikundi na Taasisi za serikali juu ya uzalishaji miche bora, upandaji na utunzaji.

**TAKWIMU ZA MITI ILIYOPANDWA WILAYA YA MBOGWE**

| NA. | MWAKA | IDADI YA MITI/MICHE ILIYOPANDWA |
|---|---|---|
| 1. | 2015/16 | 155,336 |
| 2. | 2016/17 | 323,430 |
| 3. | 2017/18 | 249,975 |
| 4. | 2018/19 | 537,050 |
| 5. | 2019/20 | 254,200 |
| **Jumla** | | **1,519,991** |

**ii. Utatuzi Wa Migogoro kati ya Hifadhi na Vijiji Jirani**

Katika Kutatua Kero ya Kimipaka Kati ya Hifadhi Pamoja na Vijiji jirani na Hifadhi, Jumla ya Vigingi (Beacons) saba (**7**) vilisimikwa katika Msitu wa Mkweni Kwa upande wa Vijiji vya **Budoda, Nyakasaluma, Bukandwe, Kanegere Mlimani** na **Kabanga**. Pia Vibao vyenye katazo la shughuli zisizoruhusiwa hifadhini jumla ya kumi na tano (**15**) vilisimikwa katika maeneo mbalimbali ya Msitu na hivyo kupunguza Migogoro kati ya Hifadhi na Wananchi.

### 3.2.4 WAKALA WA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJIJINI (RUWASA)

Ibara ya 54 (a) ya ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 inasema Kuboresha huduma ya maji vijijini kutoka asilimia 53.4 mwaka 2015 hadi asilimia 70 mwaka 2020. Wilaya ya Mbogwe katika kutekeleza ibara hii imetekeleza kama ifuatavyo:

Katika kipindi cha mwaka 2015-2019 ikiwa inafahamika kama Idara ya Maji Wilaya na kuanzia Julai, 2019-2020 baada ya kuanzishwa kwa Sheria ya Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira, Na.5 ya mwaka 2019 ilipelekea kuanzishwa kwa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) na imeendelea na usimamizi wa ujenzi wa miundombinu mipya ya maji, ukarabati wa visima, upanuzi wa miradi ya maji na kuendelea kutafuta vyanzo vipya vya maji ili maeneo ambayo hayajafikiwa na huduma ya maji wapate huduma hiyo.

Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012 Wilaya ya Mbogwe ilikuwa na wakazi wapatao 193,922, hata hivyo kwa sasa inakadiliwa idadi hiyo imeongezeka na kufikia wakazi wapatao 258,460 kwa mujibu wa takwimu zilizofanyiwa na maoteo na NBS mwaka 2019. Aidha, upatikanaji wa huduma ya maji Wilayani wakazi wapatao 114,992 sawa na asilimia 52 ya wakazi wote wanapata huduma ya maji safi na salama. Wananchi wa Wilaya ya Mbogwe wanapata huduma ya maji kutoka katika vyanzo mbalimbali ambavyo ni visima vifupi, visima virefu, skimu za maji na matenki ya kuvuna maji ya mvua, vyanzo hivi sio vya uhakika na hukauka wakati wa kiangazi.

Shughuli zilizofanyika katika kipindi cha 2015-2020 ni kama ifuatavyo:

i. Uchimbaji wa visima virefu (13) umefanyika katika Vijiji vya Shinyanga A (2), Lugunga (1), Ilolangulu (1), Iponya (2), Bugalagala (1), Iboya (1), Kabanga – Nhomolwa (1), Bugalagala (1), Ushirika (1), Nanda (1) na Bwelwa (1) na gharama zilizotumika kwa kazi husika ni Tshs. 232,373,455.00.

ii. Upanuzi wa Mradi wa Maji Nyakafuru (Kwa kujenga nyumba ya mtambo, Ununuzi wa jenereta na ulazaji wa bomba za njia kuu 3.2KM) zenye gharama ya Tshs. 94,823,194.00.

iii. Ujenzi wa vituo saba vya kuchotea Maji umekamilika katika Miradi ya Maji Nyakafuru (3), Shenda-Masumbwe (1) na Lulembela (3) vyenye gharama ya Tshs. 31,161,500.00.

iv. Kati ujenzi wa mradi wa maji wa Kabanga-Nhomolwa vituo vya kuchotea maji 18 vimekamilika, Ujenzi wa bomba na uezekaji wa nyumba ya mtambo umekamilika, ufyatuaji wa tofali za kujengea matenki (2) umekamilika, ujenzi wa tenki la kuhifadhia maji katika kijiji cha Kabanga na Nhomolwa unaendelea.

Gharama ya mkataba wa ujenzi ni Tshs. 1,239,808,334.8 ambapo hadi sasa mkandarasi hajaomba kulipwa fedha zozote kwa kazi alizofanya.

v. Ufungaji wa nishati ya umeme katika Miradi ya Maji Shenda-Masumbwe, Lulembela na Nyakafuru Tshs. 131,627,678.4.

vi. Ujenzi wa sakafu (3) na ununuzi wa pampu za mkono visima virefu 6 ufungaji wa pampu katika vijiji vya Iponya (1), Masumbwe (1) na Ushirika (1) umekamilika. Shughuli ya kufunga Pampu na kujenga sakafu katika visima vitatu bado haijakamilika. Visima hivyo vipo katika Vijiji vya Bulugala, Ilolangulu na Bagalagala gharama iliyotumika kwa kazi hiyo ni Tshs. 10,740,500.00.

vii. Ununuzi wa Pampu (12), Vipuri 75 za visima vifupi na Ukarabati wa sakafu za visima 87 katika kata 17 katika vijiji vya Kakumbi, Luhala, Mlange, Kasaka, Nyasato, Ushirika, Mlale, Bukandwe, Kanegere, Maguta, Nhungwiza, Lubeho, Ilolangulu, Mubamba,Kanangwe, Kiseke, Busabaga, Bugalagala, Kagongo, Iponya na Kabanga (Nhomolwa) gharama ya Tshs. 46,319,561.60 imetumika.

viii. Upembuzi yakinifu na usanifu wa miradi ya maji Mbogwe, Lulembela, Nyakafuru na Shenda-Masumbwe umekamilika na ripoti zimekwisha wasilisha Wizarani ili kupata kibali cha kujenga miradi hiyo. Aidha, mradi wa Mbogwe hatua iliyofikiwa ni kusimika nguzo za umeme hadi katika eneo litakalojengwa nyumba ya mtambo, tofali 670 zimefyatuliwa kwa ajili ya ujenzi wa tenki la kuhifadhia maji katika mradi wa maji mbogwe.Vilevile kwa mradi wa maji Shenda- Masumbwe kituo kimoja cha kuchotea maji kimejengwa na kinatoa huduma na mpango uliopo ni kuongeza vituo vingine vinne (4) katika vitongoji vya Lugito, Kibondo "A", Kibondo "B" na Itarike Magharibi.

ix. Utafiti wa njia kuu ya bomba na njia ya usambazaji, kuainisha maeneo ya kujenga matenki na vituo vya kuchotea maji katika Vijiji 17 ambavyo ni Kagera, Lulembela, Kashelo, Bugalagala, Ilolangulu, Nanda, Kasosobe, Ushirika, Bunigonzi, Ngemo, Isebya, Isungabula, Lugunga, Shinyanga A & B, Masumbwe, Iponya na Nyanhwiga umekamilika.



**UJENZI WA TENKI LA MAJI KABANGA KATIKA MRADI WA MAJI KABANGA-NHOMOLWA**



**MRADI WA KISIMA KIREFU CHA MAJI KIJIJI CHA BUKANDWE**



**KISIMA KIFUPI MCHANGANI KILICHOPO KATIKA KIJIJI CHA MLALE KATA YA USHIRIKA KABLA YA UKARABATI.**




**KISIMA KIFUPI MCHANGANI KILICHOPO KATIKA KIJIJI CHA MLALE KATA YA USHIRIKA KABLA YA UKARABATI**





**MRADI WA KISIMA KIFUPI CHA MAJI KAKUMBI**

## 4.0 FURSA ZA UWEKEZAJI WILAYA YA MBOGWE

Wilaya ya Mbogwe inazo fursa nyingi za uwekezaji ambazo endapo zitatumika vizuri zinaweza kuongeza kipato cha wananchi wa Wilaya ya Mbogwe na kubadilisha kabisa hali yao ya maisha sambamba na azma ya Serikali ya Awamu ya Tano kuwa na Uchumi wa Kati ifikapo mwaka 2025. Aidha, ni ukweli usiopingika kuwa maendeleo ya Jamii yoyote ile yana mahusiano makubwa na kiasi cha raslimali zilizopo na namna jamii hiyo inavyoweza kuzitumia raslimali hizo.

### 4.1 Mpango Mkakati wa Uendelezaji Viwanda – Maeneo yaliyotengwa, kupimwa na kulipiwa fidia;

Wilaya ya Mbogwe ilifanikiwa kupima/kutenga maeneo kwa ajili ya uendelezaji wa viwanda ekari 480.9 katika kata za Bukandwe na Lubeho kati ya hizo hakuna eneo lililolipiwa fidia, hata hivyo Halmashauri inawaelekeza wawekezaji kulipa fidia ya eneo wanalolihitaji badala ya kusubiri Serikali. Huu ni utekelezaji wa maagizo ya serikali yanayotaka kila Wilaya kutenga maeneo katika kata na vijiji kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vidogo na vya kati hali itakayopelekea Tanzania kutimiza ndoto ya kuwa nchi yenye Uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

### 4.2 Fursa za Uwekezaji zilizopo katika Wilaya ya Mbogwe ni kama ifuatavyo:

#### 4.2.1 Sekta ya Kilimo na Ushirika

Zaidi ya asilimia 90 ya wakazi wa Wilaya ya Mbogwe hujishughulisha na kilimo cha mazao ya biashara na chakula kama shughuli yao kuu ya kiuchumi. Wilaya ina jumla ya eneo lenye ukubwa wa $km^2$2, 394.91 Kati ya hizo Ha.191, 909, eneo linalolimwa ni Ha. 153,523 zinatumika kwa kilimo sawa na asilimia 80.0 ya eneo linalofaa kwa kilimo, aidha, ardhi ina rutuba na hali ya hewa ni nzuri ikiwemo mvua za kutosha kustawisha mazao ya chakula na biashara ya aina mbalimbali. Aidha, Wilaya ina mpango wa kujenga skimu ya umwagiliaji katika Kata ya Isebya ambapo kuna Ha. 60 zitakazotumika kulima mpunga, hivyo fursa zilizopo katika sekta hii ni kama ifuatavyo:

| NA | AINA YA FURSA | ENEO |
|---|---|---|
| 1. | Kilimo cha zao la Pamba | Kata zote 17 |
| 2. | Kilimo cha zao la Karanga | Kata zote 17 |
| 3. | Kilimo cha zao la Alizeti | Kata zote 17 |
| 4. | Kilimo cha Mahindi | Kata zote 17 |
| 5. | Kilimo cha Mpunga | Kata zote 17 |
| 6. | Kilimo cha Dengu | Kata ya Lugunga, Bukandwe na Nhomolwa |
| 7. | Kilimo cha Mboga mboga, maua na matuda | Kata zote 17 |
| 8. | Ujenzi wa maghala ya kisasa | Masumbwe, Lulembela na Bugalagala |
| 9. | Ujenzi wa viwanda vya kuongeza thamani mazao – kukamua mafuta ya mbegu, kutengeneza nguo na kusindika matunda | Kata zote 17 |

### 4.2.2 Sekta ya Mifugo na Uvuvi

Sekta ya Mifugo na Uvuvi ni moja kati ya sekta zinazopewa umuhimu mkubwa katika kukuza na kupunguza umasikini nchini, aidha ni moja kati ya shughuli muhimu katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe. Inakadiriwa kuwa Zaidi ya asilimia 70 ya wakazi wote wanajishughulisha na ufugaji wa mifugo mbalimbali kwa lengo la kujipatia lishe, kipato na pia ni benki hai kwa wafugaji hasa kipindi cha kiangazi. Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe inakadiriwa kuwa na mifugo ya aina mbalimbali kama ng`ombe wa asili 185,410, ng`ombe wa kisasa 81, mbuzi 76,843, kondoo 41,850, nguruwe 27,423, kuku wa asili 276,315, kuku wa kisasa 18,700 na wengineo. Mifugo hii ni sehemu ya chakula muhimu aina ya protein na mingine inatumika kama wanyama kazi wa kulima na kubeba mizigo. Aidha, Wilaya ya Mbogwe inazalisha maziwa ya ng`ombe wastani wa lita 44,400 kwa mwezi na nyama ya ng`ombe kg 9,750 kwa mwezi, maziwa yanahitajika kukusanywa katika vituo vya kukusanyia maziwa, kuchakatwa na kuhifadhiwa vizuri kwa matumizi ya binadamu. Uwekezaji katika Sekta hii utaboresha mifugo inayofugwa ili iweze kutoa mazao mengi na bora, hivyo kuongeza kipato cha mwananchi. Fursa zilizopo katika Sekta hii ni kama ifuatavyo:

| NA | AINA YA FURSA | ENEO |
|---|---|---|
| 1. | Kunenepesha mifugo | Kata za Masumbwe na Nyakafuru |
| 2. | Kujenga kituo/kiwanda cha kuchakata na kusindika mazao yatokanayo na mifugo ili kuyaongezea thamani – maziwa, nyama, ngozi na mayai | Lubeho, kata ya Nyakafulu |
| 3. | Kujenga kiwanda cha kusindika vyakula vya mifugo | Lubeho, kata ya Nyakafulu |
| 4. | Kujenga kiwanda cha kuzalisha mbegu bora za malisho ya mifugo | Lubeho, kata ya Nyakafulu |
| 5. | Kujenga mnada wa kisasa wa mifugo | Kata za Masumbwe na Nyakafulu |

### 4.2.3 Sekta ya Madini

Wilaya ya Mbogwe ipo katika Ukanda wa Madini hasa Dhahabu inayochimbwa na wachimbaji wadogo wadogo ambao hawana utaalamu wala vifaa vya kisasa vya kuchimbia na kuchenjua dhahabu, hii inapelekea kuchimba kina kifupi na kupoteza dhahabu wakati wa kusafisha. Hivyo, tunawahitaji wawekezaji wenye utaalamu wa kutosha na vifaa vya kisasa watakao fanya utafiti wa kutosha na wa kina ili kujua kiasi na aina ya madini kilichopo hii itatoa uhakika kwa wawekezaji kuwa watafanya kazi ya faida na sio ya hasara, hasa ukizingatia kuwa uwekezaji katika uchimbaji wa madini unahitaji mtaji mkubwa. Halmashauri inahitaji wawekezaji wenye utaalamu wa madini kutosha na wenye mtaji wa kufanya utafiti juu ya kiasi na aina ya madini yaliyopo hii itaongeza usalama, kiasi kinachochimbwa, ubora wa madini yatakayochimbwa, hii itaongeza kipato cha wachimbaji, pato la Halmashauri na Serikali kwa jumla.

Katika Halmashauri ya Wilaya, viwanda vya uchenjuaji wa dhahabu kwa kutumia teknolojia ya V.A.T leaching vimeongezeka kutoka 12 mwaka 2015 hadi 36 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 200. Pia, Soko la dhahabu limeanzishwa, sawa na mafanikio ya asilimia 100 ya kuanzisha soko la dhahabu kila wilaya.

| NA | AINA YA FURSA | ENEO |
|---|---|---|
| 1. | Uchimbaji wa Dhahabu | Nyakafuru, Bukandwe, Shenda, Kakumbi |
| 2. | Viwanda vya kuchenjulia Dhahabu | Nyakafuru, Bukandwe, Shenda, Kakumbi |
| 3. | Viwanda vya kutengeneza bidhaa zitokanao na dhahabu – pete, mikufu, kung`arisha vitu mbalimbali | Kata ya Masumbwe |

**PICHA ZA UWEKEZAJI KATIKA SEKTA YA MADINI**




**UJENZI WA KIWANDA CHA KUCHENJUA DHAHABU KIJIJI CHA BUKANDWE**



**UJENZI WA KIWANDA CHA KUCHENJUA DHAHABU (KAHAMA GROUP TANZANIA LTD) KIJIJI CHA SHENDA**




**SOKO LA DHAHABU MBOGWE**

### 4.2.4 Sekta ya Elimu

Wilaya ya Mbogwe ina jumla ya shule 89 za Msingi kati ya hizo 84 za Serikali na 5 za watu binafsi na shule 13 za sekondari za kidato cha I & IV zote za Serikali. Wilaya haina shule za sekondari za kidato cha V & VI wala vyuo vya aina yoyote, hali inayopelekea wananchi kutafuta huduma hii nje ya Wilaya ya Mbogwe. Tuna wahitaji wawekezaji katika Sekta hii watakaojenga shule za kidato cha V & VI za kisasa na vyuo vya ufundi/VETA ili kuwaandaa vijana wetu kuwa na ujuzi na maarifa ya kutumia raslimali zinazotuzunguka kwa manufaa yao na nchi kwa ujumla, raslimali nyingi kwa sasa aidha hazitumiki (not utilized) au zinatumika chini ya kiwango (under utilized) au zinatumika visivyo (mis utilized).

### 4.2.5 Sekta ya Afya

Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe ilianzishwa mwaka 2012 baada ya kuigawa Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe, hivyo bado haina miundombinu ya kutosha ikiwemo Hospitali ya Wilaya.

Aidha katika kata 17 ni kata 2 tu ndizo zina Vituo vya Afya na katika Vijiji 87 ni Vijiji 14 tu vina zahanati. Upungufu huu mkubwa wa vituo vya kutolea huduma za Afya una wafanya wananchi wa Wilaya ya Mbogwe hupoteza muda mwingi na kutembea umbali mrafu kutafuta huduma za Afya, muda ambao ungeweza kutumika kuzalisha mali.

Wilaya ya Mbogwe inawahitaji wawekezaji watakaojenga miundombinu ya kutolea huduma za Afya na kuwapunguzia wananchi adha ya kusafiri mwendo mrefu kuitafuta huduma hiyo.

### 4.2.6 Sekta ya Ardhi na Maliasili

Wilaya ya Mbogwe inapakana na misitu mingi ya asili na Mapori Tengefu ya Hifadhi likiwemo pori la Kigosi/Moyowosi na Vilima vya Mkweni ambapo kuna miti mingi ya asili inayotoa maua yanayowavutia nyuki kupata chakula chao na hatimaye kutengeneza asali yenye ubora kwa matumizi ya binadamu ambapo matokeo ya sampuli ya asali iliyowasilishwa kwa Mkemia Mkuu wa Serikali imethibitishwa kuwa na ubora unaokidhi viwango vya Kimataifa. Wilaya inamhitaji mwekezaji atakayewekeza kwenye ufugaji wa nyuki kwa kiwango kikubwa na kujenga kiwanda cha kuchakata asali.

Takwimu za hadi Juni, 2018 zinaonesha kuwa uzalishaji wa asali kwa kutumia mizinga ya kisasa unatoa kg 20 – 27 za asali, na bei kwa sasa ni Tsh. 8,000/= - 10,000/= kwa kg na kwamba soko la asali ni la uhakika, nta inauzwa kwa bei ya Tsh. 10,000/= - 15,000/= kwa kg.

Uwekezaji katika ufugaji wa nyuki utasaidia kuhifadhi mazingira hivyo, kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi pia ufugaji wa nyuki unasaidia kuchavusha mimea inayotoa maua. Hii itapelekea mwananchi mmoja mmoja kuhamasika na kuanza kufuga nyuki kwa njia bora na kuongeza uzalishaji wa asali na hatimaye kipato cha kaya na nchi kwa ujumla. Misitu ya asili katika Wilaya ya Mbogwe imeharibiwa kwa kiasi kikubwa na shughuli za kibinadamu – kilimo, ufugaji, ujenzi wa makazi, nishati ya kuni na mkaa na matumizi mengineyo, hivyo upandaji wa miti kibiashara kwa kutumia mbegu za asili na za kigeni utasaidia kurudisha uoto wa asili lakini pia kuongeza kipato kutokana na mauzo ya mazao ya misitu kama mbao, nguzo na kujengea na mengineyo.

| NA | AINA YA FURSA | ENEO |
|---|---|---|
| 1. | Kufuga Nyuki wa Asali, kuchakata na kusindika mazao yatokanayo na nyuki – asali, nta na kutoa ajira kwa jamii | Kata ya Iponya na Iboya |
| 2. | Hifadhi ya Mazingira | Kata ya Iponya na Iboya |
| 3. | Kupanda miti kibiashara | Kata za Lugunga, Lulembela |

### 4.3 Mwitikio wa wawekezaji:

(i) Benki ya NMB - Masumbwe
(ii) Benki ya CRDB - Masumbwe
(iii) Robert Msompola – Kiwanda cha kuongeza thamani ya zao la Mpunga na Karanga - Masumbwe
(iv) Jehovah Rapha (JR) – Kiwanda cha kuongeza thamani ya zao la Mpunga na Karanga - Masumbwe
(v) Shanks Tumbulizo – Kiwanda cha kuongeza thamani ya zao la Mpunga na Karanga - Masumbwe
(vi) Hadija – Kiwanda cha kuongeza thamani ya zao la Mpunga na Karanga
(vii) Ragaa Alfady Group Of Company - Kiwanda cha Kuchenjua Dhahabu – Bukandwe
(viii) Kahama Group Tanzania Ltd - Kiwanda cha Kuchenjua Dhahabu – Shenda

## PICHA ZA UWEKEZAJI KATIKA SEKTA ZA TAASISI ZA KIBENKI




**UJENZI WA BENKI YA CRDB WILAYA YA MBOGWE**




**HUDUMA ZA BENKI YA NMB WILAYA YA MBOGWE**





**GHALA LA KUHIFADHIA MAZAO NA MASHINE ZA KUKOBOA MPUNGA – JEHOVAH RAPHA (JR) RICE MILLS KIJIJI CHA NYAKAFULU**



**MUONEKANO WA HATUA YA UJENZI WA OFISI YA MKUU WA WILAYA YA MBOGWE**